
LAANA YA PANDU

Godfrey Nyasulu



EAST AFRICAN LITERATURE BUREAU

EAF PAM PA

Laana ya Pandu

Elimu ni kama taa ikuangazayo usiku,
Uzidipo kuipata nayo huongeza mwanga;
Ukaona ngazi ya maendeleo kati ya msitu,
Ukaipanda kwa urahisi bila kutangatanga;
Ukayafaidi matunda ya ustaarabu kila siku.

Haraka mbaya mwanga ukiwa hafifu,
Usitamani kuruka ngazi kama kipanga,
Utateleza ukaanguka na kuwa dhaifu,
Kama una bahati kutoliwa matanga,
Mwanga mdogo wataka uvumilivu na uangalifu.

Ujinga ni giza nene likuzingatialo hata juani;
Ukashindwa kuelewa, kama mtoto mchanga;
Usijue karibu yako pana hatari gani;
Dunia ikakufunika kama ganda la karanga;
Ole wao walio gizani; yawapatayo hayana mizani.

Godfrey Nyasulu

July, 1973

SURA YA KWANZA

Laana ya Pandu

Pandu alimsaidia punda wake kwa kusukuma mkokoteni mbele yake kwa nguvu. Misuli ya miguu, mikono, na kifua chake ilituna na kuonyesha ugumu kama jiwe. Mdomo wake ukiwa wazi alihema na kupumua pumzi nzito ya mchoko. Mkokoteni haukuwa mzito kwa ajili ya nazi nyingi alizopakia bali kwa sababu ya magurudumu yake ya mbao yaliyokuwa na mviringo kama mayai, na ambayo yalitowa kelele nyingi za mikwaruzo kwa ajili ya kukosa mafuta kila hatua aliyotupa ilikuwa ni kazi ya pekee. Matone mengi ya jasho yalitiririka usoni kwake na kudondokea kifuani yakalowanisha kabisa fulana yake. Mbele ya mkokoteni punda alihema na kupanua pua zake zilizotoa pumzi kama apigae chafya. Toka asubuhi alipokwenda kwenye kiunga chake cha nazi sasa ndio alikuwa akirudi nyumbani. Jua lilikuwa karibu kuzama. Lilionekana jekundu kama mpira wa moto juu ya miti iliyoonekana midogo mbali milimani.

Alipoona kuwa mkokoteni unakwenda kwa haraka, alijua kuwa sasa ameipita ile sehemu mbaya ya njia. Aliachilia mkokoteni akapiga hatua za haraka na kumtekenya mbavuni punda ambae alianza kukimbia. Pandu aliufuatia mkokoteni huku akiimba kidogo kidogo. Harufu nzuri ya mikorosho; iliyopandwa na baba yake mzee Mavuto kando kando ya barabara wakati yeye yungali mtoto; ilielea hewani na kumburudisha kama harufu ya sigara imburudishayo mvutaji. Bila kuonyesha mchoko aliendelea kuimba huku akifuta jasho usoni kwa kitambaa alichotoa mfukoni mwake. Nazi mbili zilidondoka, ikiwa ni mara ya tatu kudondoka kwa